



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA**

**BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA**



**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA KATIKA  
MSIMU WA KOROSHO 2021/2022**

**APRILI 2022**

## YALIYOMO

<b>1.0. UTANGULIZI.....</b>	<b>1</b>
1.1. Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala .....	1
1.2. Ghala Zilizopatiwa Leseni .....	1
<b>2.0. UKUSANYAJI NA UTOAJI KOROSHO GHALANI .....</b>	<b>3</b>
2.1. Ukusanyaji Korosho Ghala Kuu .....	3
2.1. Utoaji Korosho Ghala Kuu.....	4
2.2. Bei na Mapato .....	6
<b>3.0. HALI YA UTENDAJI WA WADAU MBALIMBALI .....</b>	<b>7</b>
3.1. Wakulima (Vyama vya Msingi (AMCOS)). .....	7
3.1.1. AMCOS zilizoongoza kwa makusanyo .....	7
3.1.2. AMOCS zilizoongoza kwa kukusanya Daraja la Kwanza .....	7
3.1.3. AMOCS zilizoongoza kwa mapato ya korosho .....	8
3.2. Wanunuzi .....	8
3.2.1. Wanunuzi walioongoza kununua kiasi cha korosho .....	8
3.2.2. Wanunuzi walioongoza kwa wastani wa juu wa bei.....	8
3.2.3. Ufanisi wa wanunuzi kutoa mizigo ghalani .....	9
3.3. Waendesha Ghala .....	9
<b>4.0. CHANGAMOTO .....</b>	<b>12</b>
4.1. Waendesha Ghala Kutakiwa Kutoa Korosho Kama Walivyopokea: .....	12
4.1.1. Chimbuko .....	12
4.1.2. Visababishi vya upungufu wa uzito ghalani .....	13
4.1.3. Mapendekezo .....	14
4.2. Changamoto Nyingine.....	15


## 1.0. UTANGULIZI

### 1.1. Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala

**WRRB** ni taasisi chini ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara iliyoungwa kwa Sheria Namba 10 ya 2005 na Marekebisho Kifungu **4 Sura 339 R.E. 2016** iliropewa majukumu chini ya **Kifungu 5 (a-j)** ikiwemo kutoa leseni kwa waendesha ghala, meneja dhamana na wakaguzi wa ghala; kuchapa na kuidhinisha vitabu vya Stakabadhi za Ghala, kusajili na kuingiza taarifa za wadau muhimu wa mfumo, kuwakilisha nchi katika masuala ya taifa na kimataifa yahusuyo Mfumo wa Stakabadhi za Ghala pamoja na majukumu mengine kama taasisi itakavyoelekezwa na Mhe. Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

### 1.2. Ghala Zilizopatiwa Leseni

Katika Msimu wa Korosho Mwaka 2021/2022 Bodi ilitoa jumla ya leseni za kuendesha **Ghala Kuu 34** kwa kampuni za **Waendesha Ghala 22** zilizofanya kazi katika **mikoa 6** inayozalisha korosho ikiwemo Lindi (**9**), Mtwara (**14**), Pwani (**6**), Ruvuma (**3**), Morogoro (**1**) na Tanga (**1**) inayojumuisha **wilaya 18** kama inavyoonekana katika *Kielelezo na Jedwali Na.1* hapo chini.



**Kielelezo Na.1: Mikoa yenye Ghala Kuu za Korosho Msimu 2021/2022**

## Jedwali Na.1: Ghala Kuu za Korosho 2021/2022

N	Ghala	Kampuni ya Mwendesha Ghala	Mkoa	Wilaya
1	Tanroads Nangurukuru-Kilwa	Demuton Tanzania Ltd	Lindi	Kilwa
2	Buco Holdings Ltd	Nangomba Holding Co Ltd	Lindi	Lindi
3	Lindi Farmers Limited-Mtama	Yuha Company Limited	Lindi	Lindi Vijijini
4	Hassan Yasini Mpako-Liwale	Zuma Cargo Transport Company Limited	Lindi	Liwale
5	Umoja Amcos Ltd	Kiibale Company Ltd	Lindi	Liwale
6	Lindi Farmers Limited-Nachingwea	Ahn & Raka Company Ltd	Lindi	Nachingwea
7	Nachingwea Dc	Nachingwea Investment And Supplies Ltd	Lindi	Nachingwea
8	Export Nachingwea Co. Ltd	Zuma Cargo Transport Company Limited	Lindi	Nachingwea
9	Ruangwa Dc-Plot No 4 Block A Lipande	Ruangwa Warehousing Company Ltd	Lindi	Ruangwa
1	African Ginning Ltd-Mtandi Masasi	Daywinry Company Ltd	Mtwara	Masasi
2	Mamcu Ltd - Mtandi Investors Area-Masasi	Jasaya General Trading Co Ltd	Mtwara	Masasi
3	Micronix System Ltd - Masasi Urban Area	Splendors Control Ltd	Mtwara	Masasi
4	Perfect Cashew Kernel(T) Ltd-Mtandi Investors Area	Perfect Cashew Kernel Ltd	Mtwara	Masasi
5	Rashid Seleman Rashid	Daywinry Company Ltd	Mtwara	Masasi
6	Cashewnut Company Ltd (2005)	Kejuliana Co Ltd	Mtwara	Mtwara
7	Mamcu Ltd - Nanyamba	Rahami Agri.Investment Limited	Mtwara	Mtwara
8	Kenoshukuru Mangaka	Chilindo Company Limited	Mtwara	Nanyumbu
9	Mamcu Ltd - Ndwiki Village - Nanyumbu	L. M. Malegeri Co Ltd	Mtwara	Nanyumbu
10	Mohamed Kossa Abdallah-Nanyumbu	Kossa Company Limited	Mtwara	Nanyumbu
11	Micronix Systems Ltd - Newala Urban Area	Splendors Control Ltd	Mtwara	Newala
12	Tanecu Ltd-Agrofocus-Newala	Partner General Supplies	Mtwara	Newala
13	Tanecu Ltd - Newala	L. M. Malegeri Co Ltd	Mtwara	Newala
14	Tanecu Ltd - Tandahimba	Ngonde Traders Company Limited	Mtwara	Tandahimba
1	Misugusugu	Pisah Limited	Pwani	Kibaha
2	Corecu (1984) Ltd- Kibiti A	I&R Agribusiness Company Ltd	Pwani	Kibiti
3	Juma Ally Ngwaya - Bungu	Pugna Agrifood Tanzania Ltd	Pwani	Kibiti
4	Ali Majid Nassoro-Mivule - Mkuranga	Pisah Limited	Pwani	Mkuranga
5	Hamisi Ally Likota - Muhoro	Pisah Limited	Pwani	Rufiji
6	Saidi Omari Mtulia - Ikwiriri	Pisah Limited	Pwani	Rufiji
1	Ibrahim Mohammed Ibrahim	Kossa Company Limited	Ruvuma	Tunduru
2	Tamcu Ltd	Daywinry Company Ltd	Ruvuma	Tunduru
3	Fuad Abdallah Said	Zuma Cargo Transport Company Limited	Ruvuma	Tunduru
1	Kivukoni	Ngonde Traders Company Limited	Morogoro	Ulanga
1	Mohamed Salim-Tanga Tc	Demuton Tanzania Ltd	Tanga	Tanga CC

## 2.0. UKUSANYAJI NA UTOAJI KOROSHO GHALANI


Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2022, Ghala Kuu 33 kati ya 34 zilikuwa zimekamilisha zoezi la kuingiza na kutoa Korosho isipokuwa Ghala Kuu la Mkoani Tanga ambapo msimu ulikuwa unaendelea. Hivyo, takwimu zilizoanishwa hapo chini ni kamilifu kwa Ghala 33 zilizoko mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani na Morogoro; takwimu za Ghala la Tanga zilizotumika ni zile za mzigo wote uliopokelewa na kutolewa mpaka kufikia taarifa hii ilipoandaliwa

### 2.1. Ukusanyaji Korosho Ghala Kuu

Ukusanyaji wa Korosho katika Ghala Kuu chini ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala hadi kufikia tarehe 31 Machi 2022 ulifikia jumla ya **tani 231,101.851** kwa nchi nzima. Kimkoa zilikuwa zimekusanywa Lindi (**tani 65,812.861**), Mtwara (**tani 125,958.775**), Pwani (**tani 13,218.914**), Ruvuma (**tani 25,316.030**), **Morogoro (tani 137.080)** na Tanga (**tani 658.191**) (*Jedwali na Kielelezo Na. 1*).

Katika makusanyo hayo **tani 222,910.172** sawa na **96%** ya Korosho yote chini ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ilikusanywa kama **Daraja la Kwanza** na **tani 8,191.679** sawa na **4%** pekee ilikusanywa kama **Daraja la Pili**. Kwa uwiano wa kiasi cha Korosho kilichokusanywa katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala **Ruvuma na Morogoro** zinaongoza kwa kuwa na **100%** ya Korosho Daraja la Kwanza; ikifuatiwa na **Lindi 99%**, **Mtwara 97%**, **Tanga 92%** na **Pwani 70%**.

Aidha, licha ya mkoa wa Morogoro kutumia Mfumo kwa mara ya kwanza, Korosho iliyokusanywa ilikuwa **100% Daraja la I** ikilinganishwa na baadhi ya maeneo ambayo yametekeleza kwa muda. Hii inaashiria kuwa kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo mazao yanaweza kuongeza ubora na hivyo tija na bei kwa mkulima.



**Kielelezo Na.2: Ukusanyaji Korosho Ghala Kuu Msimu 2021/2022**

## Jedwali Na.2: Ukusanyaji Korosho Ghala Kuu Msimu 2021/2022

N	Ghala	Kampuni ya Mwendesha Ghala	Mkoa	Wilaya	Uzito (tani)		
					Daraja la Kwanza	Daraja la Pili	Jumla ya Korosho
1	Tanroads Nangurukuru-Kilwa	Demuton Tanzania Ltd	Lindi	Kilwa	5,861.260	81.188	5,942.448
2	Buco Holdings Ltd	Nangomba Holding Co Ltd	Lindi	Lindi	4,701.846	191.868	4,893.714
3	Lindi Farmers Limited-Mtama	Yuha Company Limited	Lindi	Lindi Vijijini	8,391.078	213.319	8,604.397
4	Hassan Yasini Mpako-Liwale	Zuma Cargo Transport Company Limited	Lindi	Liwale	707.549	33.956	741.505
5	Umaja Amcos Ltd	Kiibale Company Ltd	Lindi	Liwale	14,597.298	133.034	14,730.332
6	Lindi Farmers Limited-Nachingwea	Ahn & Raka Company Ltd	Lindi	Nachingwea	5,006.958	-	5,006.958
7	Nachingwea Dc	Nachingwea Investment And Supplies Ltd	Lindi	Nachingwea	8,180.142	-	8,180.142
8	Export Nachingwea Co. Ltd	Zuma Cargo Transport Company Limited	Lindi	Nachingwea	4,599.477	-	4,599.477
9	Ruangwa Dc-Plot No 4 Block A Lipande	Ruangwa Warehousing Company Ltd	Lindi	Ruangwa	13,113.888	-	13,113.888
	<b>Jumla ndogo Lindi</b>				<b>65,159.496</b>	<b>653.365</b>	<b>65,812.861</b>
1	African Ginning Ltd-Mtandi Masasi	Daywinry Company Ltd	Mtwara	Masasi	5,373.985	-	5,373.985
2	Mamcu Ltd - Mtandi Investors Area-Masasi	Jasaya General Trading Co Ltd	Mtwara	Masasi	15,603.187	-	15,603.187
3	Micronix System Ltd - Masasi Urban Area	Splendors Control Ltd	Mtwara	Masasi	11,046.183	-	11,046.183
4	Perfect Cashew Kernel(T) Ltd-Mtandi Investors Area	Perfect Cashew Kernel Ltd	Mtwara	Masasi	4,600.969	-	4,600.969
5	Rashid Seleman Rashid	Daywinry Company Ltd	Mtwara	Masasi	495.956	-	495.956
6	Cashewnut Company Ltd (2005)	Kejuliana Co Ltd	Mtwara	Mtwara	13,651.832	1,458.097	15,109.929
7	Mamcu Ltd - Nanyamba	Rahami Agri.Investment Limited	Mtwara	Mtwara	7,035.903	743.443	7,779.346
8	Kenoshukuru Mangaka	Chilindo Company Limited	Mtwara	Nanyumbu	3,814.320	-	3,814.320
9	Mamcu Ltd - Ndwiika Village - Nanyumbu	L. M. Malegeri Co Ltd	Mtwara	Nanyumbu	3,706.173	0.079	3,714.252
10	Mohamed Kossa Abdallah-Nanyumbu	Kossa Company Limited	Mtwara	Nanyumbu	1,523.620	-	1,523.620
11	Micronix Systems Ltd - Newala Urban Area	Splendors Control Ltd	Mtwara	Newala	8,084.266	358.009	8,442.275
12	Tanecu Ltd-Agrofocus-Newala	Partner General Supplies	Mtwara	Newala	7,626.490	181.759	7,808.249
13	Tanecu Ltd - Newala	L. M. Malegeri Co Ltd	Mtwara	Newala	6,293.217	234.832	6,528.049
14	Tanecu Ltd - Tandahimba	Ngonde Traders Company Limited	Mtwara	Tandahimba	33,600.099	518.356	34,118.455
	<b>Jumla ndogo Mtwara</b>				<b>122,456.200</b>	<b>3,502.575</b>	<b>125,958.775</b>
1	Misugusugu	Pisah Limited	Pwani	Kibaha	53.720	73.135	126.855
2	Corecu (1984) Ltd- Kibiti A	I&R Agribusiness Company Ltd	Pwani	Kibiti	3,892.027	935.999	4,828.026
3	Juma Ally Ngwaya - Bungu	Pugna Agrifood Tanzania Ltd	Pwani	Kibiti	2,475.382	827.615	3,302.997
4	Ali Majid Nassoro-Mivule - Mkuranga	Pisah Limited	Pwani	Mkuranga	738.666	1,392.575	2,131.241
5	Hamisi Ally Likota - Muhoro	Pisah Limited	Pwani	Rufiji	369.946	20.974	390.920
6	Saidi Omari Mtulia - Ikwiriri	Pisah Limited	Pwani	Rufiji	1,729.328	709.548	2,438.875
	<b>Jumla ndogo Pwani</b>				<b>9,259.068</b>	<b>3,959.846</b>	<b>13,218.914</b>
1	Ibrahim Mohammed Ibrahim	Kossa Company Limited	Ruvuma	Tunduru	6,002.254	-	6,002.254
2	Tamcu Ltd	Daywinry Company Ltd	Ruvuma	Tunduru	3,456.553	-	3,456.553
3	Fuad Abdallah Said	Zuma Cargo Transport Company Limited	Ruvuma	Tunduru	15,832.882	24.341	15,857.223
	<b>Jumla ndogo Ruvuma</b>				<b>25,291.689</b>	<b>24.341</b>	<b>25,316.030</b>
1	Kivukoni	Ngonde Traders Company Limited	Morogoro	Ulanga	137.080	-	137.080
	<b>Jumla ndogo Morogoro</b>				<b>137.080</b>	<b>-</b>	<b>137.080</b>
1	Mohamed Salim-Tanga Tc	Demuton Tanzania Ltd	Tanga	Tanga CC	606.639	51.552	658.191
	<b>Jumla ndogo Tanga</b>				<b>606.639</b>	<b>51.552</b>	<b>658.191</b>
<b>Jumla Kuu</b>					<b>222,910.172</b>	<b>8,191.679</b>	<b>231,101.851</b>


### 2.1. Utoaji Korosho Ghala Kuu

Utoaji wa Korosho katika Ghala Kuu chini ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala hadi kufikia tarehe 31 Machi 2022 katika tani **231,101.851** zilizopokelewa nchi nzima; palitokea upungufu wa tani **1,529.912** sawa na **0.66%** hivyo kufanya kiasi halisi kilichotoka kuwa sawa na tani **230,044.696** (Jedwali Na.3). Kwa kutumia utaratibu uliopo kisheria, kila upungufu uliojitokeza na kuripotiwa kupitia Fomu Namba 7; madai hayo yaliwasilishwa kwa kampuni za bima kwa ajili ya malipo. Vyanzo vina/vilivyosababisha upungufu vimeelezwa kwa kina *Sehemu ya 4.1.2.*

## Jedwali Na.3: Utoaji Korosho Ghala Kuu Msimu 2021/2022

N	Ghala	Mwendesha Ghala	Mkoa	Wilaya	Uzito (Kg)				
					Uliopokelewa (Kg)	Uliyotoka (Kg)	Tofauti (Kg)	Tofauti (%)	
1	Tanroads Nangurukuru-Kilwa	Demuton Tanzania Ltd	Lindi	Kilwa	5,942,448	5,929,716	-	12,732	-0.21%
2	Buco Holdings Ltd	Nangomba Holding Co Ltd	Lindi	Lindi	4,893,714	4,860,748	-	32,966	-0.67%
3	Lindi Farmers Limited-Mtama	Yuha Company Limited	Lindi	Lindi Vijijini	8,604,397	8,490,490	-	113,907	-1.32%
4	Hassan Yasini Mpako-Liwale	Zuma Cargo Transport Company Limited	Lindi	Liwale	741,505	739,199	-	2,306	-0.31%
5	Umoja Amcos Ltd	Kiibale Company Ltd	Lindi	Liwale	14,730,332	14,633,738	-	96,594	-0.66%
6	Lindi Farmers Limited-Nachingwea	Ahn & Raka Company Ltd	Lindi	Nachingwea	5,006,958	4,980,518	-	26,440	-0.53%
7	Nachingwea Dc	Nachingwea Investment And Supplies Ltd	Lindi	Nachingwea	8,180,142	8,089,295	-	90,847	-1.11%
8	Export Nachingwea Co. Ltd	Zuma Cargo Transport Company Limited	Lindi	Nachingwea	4,599,477	4,583,731	-	15,747	-0.34%
9	Ruangwa Dc-Plot No 4 Block A Lipande	Ruangwa Warehousing Company Ltd	Lindi	Ruangwa	13,113,888	13,053,989	-	59,899	-0.46%
<b>Sub-total Lindi</b>					<b>65,812,861</b>	<b>65,361,423</b>	<b>-</b>	<b>451,438</b>	<b>-0.69%</b>
1	African Ginning Ltd-Mtandani Masasi	Daywinny Company Ltd	Mtwara	Masasi	5,373,985	5,375,412	-	1,427	0.03%
2	Mamcu Ltd - Mtandani Investors Area-Masasi	Jasaya General Trading Co Ltd	Mtwara	Masasi	15,603,187	16,067,876	-	8,068	-0.05%
3	Micronix System Ltd - Masasi Urban Area	Splendors Control Ltd	Mtwara	Masasi	11,046,183	10,962,655	-	83,528	-0.76%
4	Perfect Cashew Kernel(T) Ltd-Mtandani Investors Area	Perfect Cashew Kernel Ltd	Mtwara	Masasi	4,600,969	4,580,068	-	20,901	-0.45%
5	Rashid Seleman Rashid	Daywinny Company Ltd	Mtwara	Masasi	495,956	495,920	-	36	-0.01%
6	Cashewnut Company Ltd (2005)	Kejuliana Co Ltd	Mtwara	Mtwara	15,109,929	14,771,181	-	338,748	-2.24%
7	Mamcu Ltd - Nanyamba	Rahami Agri.Investment Limited	Mtwara	Mtwara	7,779,346	7,726,366	-	52,980	-0.68%
8	Kenoshukuru Mangaka	Chilindo Company Limited	Mtwara	Nanyumbu	3,814,320	3,786,411	-	27,909	-0.73%
9	Mamcu Ltd - Ndwiika Village - Nanyumbu	L. M. Malegeri Co Ltd	Mtwara	Nanyumbu	3,714,252	3,688,447	-	25,805	-0.69%
10	Mohamed Kossa Abdallah-Nanyumbu	Kossa Company Limited	Mtwara	Nanyumbu	1,523,620	1,457,074	-	66,546	-4.37%
11	Micronix Systems Ltd - Newala Urban Area	Splendors Control Ltd	Mtwara	Newala	8,442,275	8,376,961	-	65,314	-0.77%
12	Tanecu Ltd-Agrofocus-Newala	Partner General Supplies	Mtwara	Newala	7,808,249	7,745,032	-	63,217	-0.81%
13	Tanecu Ltd - Newala	L. M. Malegeri Co Ltd	Mtwara	Newala	6,528,049	6,424,684	-	103,365	-1.58%
14	Tanecu Ltd - Tandahimba	Ngonde Traders Company Limited	Mtwara	Tandahimba	34,118,455	33,934,309	-	184,146	-0.54%
<b>Sub-total Mtwara</b>					<b>125,958,775</b>	<b>125,392,396</b>	<b>-</b>	<b>1,039,136</b>	<b>-0.82%</b>
1	Misugusugu	Pisah Limited	Pwani	Kibaha	126,855	126,853	-	2	0.00%
2	Corecu (1984) Ltd- Kibiti A	I&R Agribusiness Company Ltd	Pwani	Kibiti	4,828,026	4,813,053	-	14,973	-0.31%
3	Juma Ally Ngwaya - Bungu	Pugna Agrifood Tanzania Ltd	Pwani	Kibiti	3,302,997	3,291,880	-	11,117	-0.34%
4	Ali Majid Nassoro-Mivule - Mkuranga	Pisah Limited	Pwani	Mkuranga	2,131,241	2,132,631	-	1,390	0.07%
5	Hamsi Ally Likota - Muhoro	Pisah Limited	Pwani	Rufiji	390,920	388,127	-	2,794	-0.71%
6	Saidi Omari Mtulia - Ikwiriri	Pisah Limited	Pwani	Rufiji	2,438,875	2,437,933	-	942	-0.04%
<b>Sub-total Pwani</b>					<b>13,218,914</b>	<b>13,190,476</b>	<b>-</b>	<b>28,438</b>	<b>-0.22%</b>
1	Ibrahim Mohammed Ibrahim	Kossa Company Limited	Ruvuma	Tunduru	6,002,254	6,069,552	-	67,298	1.12%
2	Tamcu Ltd	Daywinny Company Ltd	Ruvuma	Tunduru	3,456,553	3,422,658	-	33,895	-0.98%
3	Fuad Abdallah Said	Zuma Cargo Transport Company Limited	Ruvuma	Tunduru	15,857,223	15,815,643	-	41,580	-0.26%
<b>Sub-total Ruvuma</b>					<b>25,316,030</b>	<b>25,307,853</b>	<b>-</b>	<b>8,177</b>	<b>-0.03%</b>
1	Kivukoni	Ngonde Traders Company Limited	Morogoro	Ulanga	137,080	136,065	-	1,015	-0.74%
<b>Sub-total Morogoro</b>					<b>137,080</b>	<b>136,065</b>	<b>-</b>	<b>1,015</b>	<b>-0.74%</b>
1	Mohamed Salim-Tanga Tc	Demuton Tanzania Ltd	Tanga	Tanga CC	658,191	656,483	-	1,708	-0.26%
<b>Sub-total Tanga</b>					<b>658,191</b>	<b>656,483</b>	<b>-</b>	<b>1,708</b>	<b>-0.26%</b>
34	<b>Grand Total</b>				<b>231,101,851</b>	<b>230,044,696</b>	<b>-</b>	<b>1,529,912</b>	<b>-0.66%</b>


Aidha, kwa kulinganisha misimu iliyotangulia kiwango cha upungufu katika Mfumo kwa ujumla kimepungua kutoka wastani wa **1.0%** (2015/2016-**1.08%**; 2016/2017-**0.97%**; 2017/2018-**0.94%**; 2019/2020-**1.09%** na 2020/2021-**0.94%**) hadi kufikia **0.66%** kama *Kielelezo Na.3* kinavyoonesha.



**Kielelezo Na.3: Mwenendo wa udhibiti wa upungufu ghalani kuanzia msimu wa mwaka 2015/2016 hadi 2021/2022**

## 2.2. Bei na Mapato

Katika msimu wa 2021/2022 Korosho iliyokusanywa na kuuzwa kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala wastani wa bei ulikuwa **Sh. 2,095.93** ambapo bei ya juu kurekodiwa ilikuwa **Sh.2,445.00** na bei ya chini **Sh.1,028.00**. Thamani ya Korosho iliyouzwa ilikuwa **Sh. Bilioni 479**. Mkoa ulioongoza kwa mapato ni mkoa wa Mtwara ulikuwa na Korosho yenye thamani ya **Sh. Bilioni 270**; ikifuatiwa na **Lindi Sh. Bilioni 134**; **Ruvuma Sh. Bilioni 50**; **Pwani Sh. Bilioni 25**; **Tanga Sh. Bilioni 1** na **Morogoro Sh. Milioni 269** (*Jedwali na Kielelezo Na.4*).



### Kielelezo Na.4: Mapato Kimkoa Msimu wa Korosho 2021/2022

#### Jedwali Na.4: Mapato na Bei Kimkoa Msimu wa Korosho 2021/2022

N	Ghala	Kampuni ya Mwendesha Ghala	Mkoa	Wilaya	Bei Iliyopatikana			Thamani
					Wastani	Juu (Max)	Chini (Min)	
1	Tanroads Nangurukuru-Kilwa	Demuton Tanzania Ltd	Lindi	Kilwa	2,042.76	2,275.00	1,601.00	12,148,151,695.00
2	Buco Holdings Ltd	Nangomba Holding Co Ltd	Lindi	Lindi	2,076.46	2,286.00	1,601.00	10,169,809,928.00
3	Lindi Farmers Limited-Mtama	Yuha Company Limited	Lindi	Lindi Vijijini	2,083.50	2,275.00	1,600.00	17,711,439,422.00
4	Hassan Yasini Mpako-Liwale	Zuma Cargo Transport Company Limited	Lindi	Liwale	1,837.07	2,231.00	1,300.00	1,382,158,157.00
5	Umaja Amcos Ltd	Kiibale Company Ltd	Lindi	Liwale	2,164.77	2,295.00	1,300.00	31,860,707,852.00
6	Lindi Farmers Limited-Nachingwea	Ahn & Raka Company Ltd	Lindi	Nachingwea	2,228.60	2,328.00	1,717.00	11,179,802,358.00
7	Nachingwea Dc	Nachingwea Investment And Supplies Ltd	Lindi	Nachingwea	2,228.97	2,330.00	1,720.00	18,267,767,436.00
8	Export Nachingwea Co. Ltd	Zuma Cargo Transport Company Limited	Lindi	Nachingwea	2,215.57	2,328.00	1,717.00	10,253,957,469.00
9	Ruangwa Dc-Plot No 4 Block A Lipande	Ruangwa Warehousing Company Ltd	Lindi	Ruangwa	2,201.31	2,328.00	1,720.00	20,526,573,567.00
<b>Jumla ndogo Lindi</b>					<b>2,119.89</b>	<b>2,330.00</b>	<b>1,300.00</b>	<b>133,500,367,884.00</b>
1	Afrisian Ginning Ltd-Mtandi Masasi	Daywinry Company Ltd	Mtwara	Masasi	2,136.47	2,320.00	1,670.00	11,621,734,801.00
2	Mamcu Ltd - Mtandi Investors Area-Masasi	Jasaya General Trading Co Ltd	Mtwara	Masasi	2,214.22	2,376.00	1,760.00	34,683,734,494.00
3	Micronix System Ltd - Masasi Urban Area	Splendors Control Ltd	Mtwara	Masasi	2,192.51	2,321.00	1,805.00	24,224,172,918.00
4	Perfect Cashew Kernel(T) Ltd-Mtandi Investors Area	Perfect Cashew Kernel Ltd	Mtwara	Masasi	2,171.18	2,331.00	1,760.00	10,010,017,886.00
5	Rashid Seleman Rashid	Daywinry Company Ltd	Mtwara	Masasi	2,260.43	2,296.00	2,200.00	1,123,246,462.00
6	Cashewnut Company Ltd (2005)	Kejiliana Co Ltd	Mtwara	Mtwara	2,043.59	2,305.00	1,200.00	30,762,340,271.00
7	Mamcu Ltd - Nanyamba	Rahami Agri.Investment Limited	Mtwara	Mtwara	1,985.55	2,400.00	1,400.00	15,559,355,079.00
8	Kenoshukuru Mangaka	Chilindo Company Limited	Mtwara	Nanyumbu	2,200.07	2,400.00	1,800.00	8,328,299,982.00
9	Mamcu Ltd - Ndwiika Village - Nanyumbu	L. M. Malegeri Co Ltd	Mtwara	Nanyumbu	2,104.05	2,296.00	1,350.00	7,912,339,252.00
10	Mohamed Kossa Abdallah-Nanyumbu	Kossa Company Limited	Mtwara	Nanyumbu	2,138.35	2,305.00	1,805.00	3,236,259,477.20
11	Micronix Systems Ltd - Newala Urban Area	Splendors Control Ltd	Mtwara	Newala	2,129.05	2,320.00	1,305.00	18,032,708,064.00
12	Tanecu Ltd-Agrofocus-Newala	Partner General Supplies	Mtwara	Newala	2,223.29	2,401.00	1,580.00	17,275,232,415.00
13	Tanecu Ltd - Newala	L. M. Malegeri Co Ltd	Mtwara	Newala	2,022.69	2,305.00	1,300.00	13,308,170,388.00
14	Tanecu Ltd - Tandahimba	Ngonde Traders Company Limited	Mtwara	Tandahimba	2,124.34	2,445.00	1,455.00	72,781,817,605.00
<b>Jumla ndogo Mtwara</b>					<b>2,138.99</b>	<b>2,445.00</b>	<b>1,200.00</b>	<b>268,859,429,094.20</b>
1	Misugusugu	Pisah Limited	Pwani	Kibaha	1,791.39	2,055.11	1,350.00	227,843,972.17
2	Corecu (1984) Ltd- Kibiti A	I&R Agribusiness Company Ltd	Pwani	Kibiti	1,906.32	2,060.00	1,250.00	9,303,292,242.50
3	Juma Ally Ngwaya - Bungu	Pugna Agrifood Tanzania Ltd	Pwani	Kibiti	1,897.85	2,057.00	1,320.00	6,304,489,643.00
4	Ali Majid Nassoro-Mivule - Mkuranga	Pisah Limited	Pwani	Mkuranga	1,772.39	2,055.00	1,250.00	3,775,146,366.90
5	Hamsi Ally Likota - Muhoro	Pisah Limited	Pwani	Rufiji	2,036.00	2,050.00	1,735.00	796,438,507.50
6	Saidi Omari Mtulia - Ikwiriri	Pisah Limited	Pwani	Rufiji	1,915.12	2,060.00	1,340.00	4,726,609,952.66
<b>Jumla ndogo Pwani</b>					<b>1,886.51</b>	<b>2,060.00</b>	<b>1,250.00</b>	<b>25,133,820,684.73</b>
1	Ibrahim Mohammed Ibrahim	Kossa Company Limited	Ruvuma	Tunduru	2,016.30	2,152.00	1,550.00	12,112,685,290.00
2	Tamcu Ltd	Daywinry Company Ltd	Ruvuma	Tunduru	2,043.07	2,170.00	1,700.00	6,987,647,846.00
3	Fuad Abdallah Said	Zuma Cargo Transport Company Limited	Ruvuma	Tunduru	1,981.36	2,160.00	1,028.00	31,320,334,355.00
<b>Jumla ndogo Ruvuma</b>					<b>2,013.57</b>	<b>2,170.00</b>	<b>1,028.00</b>	<b>50,420,667,491.00</b>
1	Kivukoni	Ngonde Traders Company Limited	Morogoro	Ulanga	2,125.33	2,270.00	1,850.00	292,763,930.00
<b>Jumla ndogo Morogoro</b>					<b>2,125.33</b>	<b>2,270.00</b>	<b>1,850.00</b>	<b>292,763,930.00</b>
1	Mohamed Salim-Tanga Tc	Demuton Tanzania Ltd	Tanga	Tanga CC	1,624.12	1,700.00	1,250.00	1,065,307,200.00
<b>Jumla ndogo Tanga</b>					<b>1,624.12</b>	<b>1,700.00</b>	<b>1,250.00</b>	<b>1,065,307,200.00</b>
<b>Wastani/Jumla Kuu</b>					<b>2,095.93</b>	<b>2,445.00</b>	<b>1,028.00</b>	<b>479,272,356,283.93</b>



### 3.0. HALI YA UTENDAJI WA WADAU MBALIMBALI

Sehemu hii inajadili utendaji wa wadau wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ikiwemo wakulima, wanunuzi na Waendesha Ghala kwa kutazama takwimu muhimu jinsi walivyofanya katika msimu wa Korosho 2021/2022.

#### 3.1. Wakulima (Vyama vya Msingi (AMCOS)).

Katika Msimu wa 2021/2022 jumla ya **AMCOS 792** zilikusanya Korosho katika Ghala Kuu mbalimbali (*Kiambatisho Na.1*). Takwimu muhimu za AMCOS hizo ni kama ifuatavyo:-

##### 3.1.1. AMCOS zilizoongoza kwa makusanyo

Kwa mujibu wa takwimu katika Kanzidata ya WRRB, **AMCOS ya Namitili** kutokea mkoa wa Ruvuma wilayani Tunduru ndiyo iliyoongoza kwa kukusanya **tani 1,879.635**; orodha ya AMCOS Kumi Bora katika makusanyo ni kama inavyoonekana katika *Jedwali Na.5*.

**Jedwali Na.5: AMCOS Kumi Bora kwa Makusanyo Msimu 2021/2022**

Nafasi	Mkoa	Wilaya	AMCOS	Jumla ya Uzito	Daraja la I	Daraja la II
1	Ruvuma	Tunduru	Namitili Amcos Ltd	1,879,635	1,879,635	-
2	Ruvuma	Tunduru	Sama Amcos Ltd	1,774,676	1,774,676	-
3	Lindi	Liwale	Umoja Amcos Ltd	1,758,118	1,719,381	38,737
4	Mtwara	Masasi	Tuaminiane Rural Primary Cooperative Society	1,656,787	1,656,787	-
5	Ruvuma	Tunduru	Lima Amcos Ltd	1,461,614	1,461,614	-
6	Mtwara	Newala	Kitangari Amcos Ltd	1,297,637	1,290,370	7,267
7	Mtwara	Nanyumbu	Mangaka Amcos Ltd	1,222,606	1,222,606	-
8	Mtwara	Masasi	Nangoo Rural Primary Cooperative Society	1,174,361	1,174,361	-
9	Pwani	Kibiti	Chapakazi Amcos Ltd	1,111,733	989,740	121,993
10	Mtwara	Mtwara	Mayanga Amcos Ltd	1,110,449	1,042,397	68,052

##### 3.1.2. AMOCS zilizoongoza kwa kukusanya Daraja la Kwanza

Kwa mujibu wa takwimu katika Kanzidata ya WRRB, **AMCOS ya Namitili** kutokea mkoa wa Ruvuma wilayani Tunduru pia, ndiyo iliyoongoza kwa kukusanya **tani 1,879.635** zilizokuwa na wastani wa **SOT ya 49.5, unyevu (MC) 7.5%** na **Idadi ya Punje (NC) 191**. Orodha ya AMCOS Kumi Bora kwa waliokusanya Daraja la I kama inavyoonekana katika *Jedwali Na.6*.

**Jedwali Na.6: AMCOS Kumi Bora kwa Daraja la I Msimu 2021/2022**

Nafasi	Mkoa	Wilaya	AMCOS	Jumla ya Uzito	Daraja la I	Daraja la II	SOT	Moisture (%w/w)	Nut Count
1	Ruvuma	Tunduru	Namitili Amcos Ltd	1,879,635	1,879,635	-	49.50	7.5	191
2	Ruvuma	Tunduru	Sama Amcos Ltd	1,774,676	1,774,676	-	49.57	7.5	183
3	Lindi	Liwale	Umoja Amcos Ltd	1,758,118	1,719,381	38,737	50.50	9.1	174
4	Mtwara	Masasi	Tuaminiane Rural Primary Cooperative Society	1,656,787	1,656,787	-	50.38	8.3	184
5	Ruvuma	Tunduru	Lima Amcos Ltd	1,461,614	1,461,614	-	49.76	7.2	184
6	Mtwara	Newala	Kitangari Amcos Ltd	1,297,637	1,290,370	7,267	51.56	9.3	180
7	Mtwara	Nanyumbu	Mangaka Amcos Ltd	1,222,606	1,222,606	-	50.47	7.2	192
8	Mtwara	Masasi	Nangoo Rural Primary Cooperative Society	1,174,361	1,174,361	-	50.75	8.7	176
9	Mtwara	Tandahimba	Matogoro Amcos Ltd	1,103,862	1,103,862	-	49.63	9.7	163
10	Mtwara	Masasi	Mporora Amcos Ltd	1,074,865	1,074,865	-	50.93	8.6	180

### 3.1.3. AMOCS zilizoongoza kwa mapato ya korosho

Kwa mujibu wa takwimu katika Kanzidata ya WRRB, **AMCOS ya Namitili** kutokea mkoa wa Ruvuma wilayani Tunduru pia, ndiyo iliyoongoza kwa kupata wastani wa thamani ya **Sh. Bilioni 3.8** katika mauzo ya Korosho Msimu 2021/2022. Orodha ya AMCOS Kumi Bora kwa mapato ni kama inavyoonekana katika *Jedwali Na.7*.

**Jedwali Na.7: AMCOS Kumi Bora kwa Daraja la I Msimu 2021/2022**

Nafasi	Mkoa	Wilaya	AMCOS	Jumla ya Uzito	Daraja la I	Daraja la II	Wastani wa Bei	Thamani (Tsh)
1	Ruvuma	Tunduru	Namitili Amcos Ltd	1,879,635	1,879,635	-	2,028.12	3,821,865,341.00
2	Lindi	Liwale	Umoja Amcos Ltd	1,758,118	1,719,381	38,737	2,136.30	3,762,810,351.00
3	Mtwara	Masasi	Tuaminiane Rural Primary Cooperative Society	1,656,787	1,656,787	-	2,132.54	3,556,821,723.00
4	Ruvuma	Tunduru	Sama Amcos Ltd	1,774,676	1,774,676	-	1,993.05	3,537,152,498.00
5	Mtwara	Newala	Kitangari Amcos Ltd	1,297,637	1,290,370	7,267	2,235.35	2,903,812,007.00
6	Ruvuma	Tunduru	Lima Amcos Ltd	1,461,614	1,461,614	-	1,987.25	2,896,818,436.00
7	Mtwara	Nanyumbu	Mangaka Amcos Ltd	1,222,606	1,222,606	-	2,101.10	2,621,289,037.20
8	Mtwara	Masasi	Nangoo Rural Primary Cooperative Society	1,174,361	1,174,361	-	2,165.64	2,549,536,362.00
9	Mtwara	Tandahimba	Matogoro Amcos Ltd	1,103,862	1,103,862	-	2,176.24	2,405,964,084.00
10	Mtwara	Masasi	Mpowora Amcos Ltd	1,074,865	1,074,865	-	2,232.92	2,401,283,377.00

### 3.2. Wanunuzi

Katika Msimu wa 2021/2022 jumla ya **Kampuni 56** za **Wanunuzi**, walijitokeza kununua na kushinda minada iliyokuwa ikifanyika kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala (*Kiambatisho Na. 2*). Takwimu muhimu za Wanunuzi hizo ni kama ifuatavyo.

#### 3.2.1. Wanunuzi walioongoza kununua kiasi cha korosho

Kwa mujibu wa takwimu katika Kanzidata ya WRRB, **Kampuni ya Sibatanza Ltd** ndiyo iliyoongoza kwa kununua **tani 30,562.108** kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Aidha, kampuni Kumi Bora zilinunua jumla ya **tani 139,404.920** sawa na **60%** ya Korosho yote iliyokusanywa kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Orodha ya Kampuni Kumi Bora kwa kiasi kilichonunuliwa ni kama inavyoonekana katika *Jedwali Na.8*.

**Jedwali Na.8: Kampuni Kumi Bora kwa kiasi cha manunuzi**

Nafasi	Jina la Mnunuzi	Lindi	Mtwara	Pwani	Ruvuma	Morogoro	Tanga	Jumla (Kg)
1	Sibatanza Limited	8,694,121	18,665,004	970,534	2,189,723	42,726	-	30,562,108
2	Export Trading Company Limited	2,707,977	11,380,922	408,173	4,704,946	-	-	19,202,018
3	Mapainia Tanzania Ltd	6,145,155	6,781,230	1,433,565	3,017,961	-	-	17,377,911
4	Iscon Commodities (T) Ltd	1,581,566	9,857,954	-	1,610,253	-	-	13,049,773
5	Tridge Tanzania Ltd	-	12,186,698	-	-	-	-	12,186,698
6	Alpha Namata Company Ltd	4,746,632	5,994,934	343,829	175,000	-	-	11,260,395
7	Udhaya Agro (T) Ltd	5,880,790	418,079	-	4,180,016	-	-	10,478,885
8	Pompous Sonthanphat Ltd	864,665	4,554,483	3,197,732	564,297	9,935	-	9,191,112
9	Kufanikiwa Tanzania Ltd	3,233,298	5,439,892	-	-	-	-	8,673,190
10	Amj Buying & Transportation Ltd	2,121,678	4,993,192	-	307,960	-	-	7,422,830
	Jumla	35,975,882	80,272,388	6,353,833	16,750,156	52,661	-	139,404,920

#### 3.2.2. Wanunuzi walioongoza kwa wastani wa juu wa bei

Kwa mujibu wa takwimu katika Kanzidata ya WRRB, **Likonde Export Co Ltd** ndiyo iliyoongoza kwa wastani wa bei ya juu kwa kutoa **Sh. 2,400.00** kwa kilo. Aidha, kampuni kumi bora kwa wastani wa bei zilitoa wastani wa **Sh. 2,291.41**

ambapo ilikuwa ni wastani wa **tani 18,450.584**. Orodha ya Kampuni Kumi Bora kwa wastani wa bei ni kama inavyoonekana katika *Jedwali Na.9*.

Aidha, wanunuzi wengi waliionekana kutoa wastani wa bei za juu kama vile CPB; walinunua kwa lengo ubanguaji; hii inaashiria kuwa uwekezaji katika ubanguaji wa ndani utaongeza tija katika bei na thamani ya zao.

### Jedwali Na.9: Kampuni Kumi Bora kwa wastani wa bei

Nafasi	Jina la Mnunuzi	Lindi	Mtwara	Pwani	Ruvuma	Morogoro	Tanga	Jumla (Kg)	Thamani (Tsh)	Wastani Bei
1	Likonde Export Company Ltd	-	96,605	-	-	-	-	96,605	231,852,000.00	2400.00
2	CPB	-	421,216	-	-	-	-	421,216	975,115,040.00	2315.00
3	Jyf Bros Enterprises Ltd	-	115,947	-	-	-	-	115,947	266,678,100.00	2300.00
4	Jegah Ltd	-	110,853	-	-	-	-	110,853	254,961,900.00	2300.00
5	Lion Agro Global Limited	63,308	795,827	-	-	-	-	859,135	1,964,714,213.00	2286.00
6	Sabari Seeds Limited	387,377	430,131	-	-	-	-	817,508	1,857,090,576.00	2271.68
7	Saisurya Export Ltd	-	236,482	-	-	-	-	236,482	536,604,970.00	2268.00
8	Tridge Tanzania Ltd	-	12,186,698	-	-	-	-	12,186,698	27,574,321,598.00	2262.21
9	Beafarm Agriventure Company	-	207,396	-	-	-	-	207,396	468,427,492.00	2258.77
10	Amago Exim Tanzania Co Ltd	1,823,049	1,485,748	-	89,947	-	-	3,398,744	7,172,956,552.00	2252.44
<b>Jumla</b>		<b>2,273,734</b>	<b>16,086,903</b>	<b>-</b>	<b>89,947</b>	<b>-</b>	<b>-</b>	<b>18,450,584</b>	<b>41,302,722,441.00</b>	<b>2291.41</b>

### 3.2.3. Ufanisi wa wanunuzi kutoa mizigo ghalani

Kwa mujibu wa takwimu katika Kanzidata ya WRRB, wastani wa mzigo kukaa ghalani tokea siku unapopokelewa mpaka mnunuzi kuuchukua ni **siku 25**. Katika msimu wa 2021/2022 kampuni ya **Jashan Agro Tanzania Ltd** ndiyo iliongoza kwa kuchukua mzigo ndani ya **siku 14** tokea kupokelewa kwake.

Muda wa mzigo kukaa ghalani hutegemea wakulima walipoanza kukusanya na kasi ya kukamilika kwa *stake* ambazo zinapofikia idadi inayotosha hupelekwa minadani; hii huweza kuchukua wastani wa siku nne hadi saba au zaidi kutegemea na eneo. Hii hufuatiwa na muda mnunuzi anaopewa kukamilisha malipo wa siku zisizopungua nne na hatimaye kuanza kutolewa pindi mnunuzi anapofika ghalani ambapo hupewa siku 14 za kazi kutoa bila adhabu.

Orodha ya Kampuni Kumi Bora kwa wastani wa siku za kutoa mzigo ghalani ni kama inavyoonekana katika *Jedwali Na. 10*.

### Jedwali Na.10: Kampuni Kumi Bora kwa ufanisi wa kutoa mzigo

Nafasi	Jina la Mnunuzi	Lindi	Mtwara	Pwani	Ruvuma	Morogoro	Tanga	Jumla (Kg)	Wastani wa Siku Ghalani
1	Jashan Agro Tanzania Limited	263,961	110,388	-	-	-	-	374,349	14
2	Ko Impex Ltd	251,328	207,801	-	-	46,477	-	505,606	15
3	Vnbp Trading Co.Ltd	1,349,999	5,657,732	-	-	-	-	7,007,731	15
4	Likonde Export Company Ltd	-	96,605	-	-	-	-	96,605	16
5	Hmedic Technology Ltd	-	-	53,614	-	-	-	53,614	17
6	Valency Agro Tanzania Ltd	612,633	591,982	-	-	-	-	1,204,615	18
7	Paradise Exim Ltd	-	262,506	502,118	-	-	-	764,624	18
8	Quality Pulse Exporters Ltd	135,568	279,713	193,489	397,265	-	-	1,006,035	18
9	Mohamed Enterprises Ltd	121,326	432,689	-	-	-	-	554,015	20
10	Ospher International Limited	1,368,243	2,098,000	-	-	-	-	3,466,243	20
<b>Wastani</b>									<b>17</b>

### 3.3. Waendesha Ghala

Katika msimu wa 2021/2022 WRRB ilitoa leseni kwa jumla ya kampuni 22 za Waendesha Ghala. Kama ilivyoatajwa katika kikao cha wadau cha tarehe 20

Julai 2021, ilipangwa katika msimu 2021/2022 Waendesha Ghala watadarajishwa kutokana na utendaji wao.

Katika udarajishaji jumla ya vigezo vikuu **vinne (4)** ambavyo ndani yake vilikuwa vimejengwa na vigezo vingine vidogo vidogo. Vigezo vilivyotumika ni kama ifuatavyo:-

- a. **Uzoefu:** Kipimo hiki kilikuwa na vigezo vinne ikiwemo **kiasi cha uzito** aliowahi kuhudumia kihistoria, **idadi ya mazao** aliyohifadhi kupitia Mfumo na **idadi ya miaka** Mwendesha Ghala aliyoko kwenye tasnia kihistoria. Kipimo hiki chote kilitumia takwimu halisi kutoka kwenye Kanzidata ya WRRB.
- b. **Hatari ya Kutengeneza Madeni:** Kipimo hiki kilikuwa na vigezo viwili ikiwemo takwimu za **kiwango cha upungufu** kilichowahi kusababishwa na Mwendesha Ghala kwa historia ya takwimu zake kwenye Mfumo na **Kinga za Utendaji** za kampuni husika zilizowasilishwa Bodi.
- c. **Malalamiko Kutoka kwa Wadau:** Kipimo hiki kilikuwa na vigezo viwili ikiwemo idadi ya malalamiko yaliyowasilishwa na kuthibitishwa kuwa na mashiko kutoka kwa **Wakulima** na **Wanunuzi**.
- d. **Uwezo wa Kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo:** Kipimo hiki kilikuwa na vigezo vitatu ambavyo vilitazama mwenendo wa Mwendesha Ghala na matukio yaliyoweza kuthibitishwa ya uvunjifu wa Sheria, Kanuni na Miongozo iliyotolewa na **WRRB, Bodi za Mazao** na au **Mamlaka za Serikali Kuu/Mitaa (Jamhuri)**.

Vigezo tajwa hapo juu vilipangwa kwa kutumia mbinu/kipimo kwa mtindo wa *Likert Scale* kwa nambari 0,1,2,3 na 4; ambapo jinsi inavyokaribia 4 ndivyo ilivyo chanya katika utendaji na jinsi inavyokaribia 0 inakuwa hasi kwa utendaji. Ufunguo wa alama ni **Hafai Kabisa** (Alama 0), **Utendaji Dhaifu** (Alama 1), **Utendaji wa Kati** (Alama 2), **Utendaji Unaoridhisha** (Alama 3), **Utendaji Uliotukuka** (Alama 4).

Kwa mujibu wa kipimo hicho, kama inavyoonekana *Jedwali Na.11* kampuni zilizoongoza ni kampuni ya **Nangomba Holding Co Ltd** iliongoza kwa ufanisi kwa kupata jumla ya **alama 3.42** na kushika nafasi ya kwanza, ikifuatia nafasi ya pili **Ngonde Trader Co Ltd** alama **3.21** na nafasi ya tatu **Perfect Cashew Kernel Ltd** alama **3.17**.

Kampuni zilizofanya kazi kwa udhaifu ni kampuni ya **Yuha Co Ltd** iliyopata **alama1.29** iliyokuwa ya mwisho, **Chilindo Co Ltd** alama **1.38** ya pili kutoka mwisho na **Partner General Supplies** alama **1.58**.

**Jedwali Na.11: Udarajishaji wa Utendaji wa Waendesha Ghala**

<b>Nafasi</b>	<b>Kampuni ya Mwendesha Ghala</b>	<b>Alama kati ya 4</b>
1	Nangomba Holding Co Ltd	3.42
2	Ngonde Traders Company Limited	3.21
3	Perfect Cashew Kernel Ltd	3.17
4	Ruangwa Warehousing Company Ltd	3.13
5	Zuma Cargo Transport Company Limited	3.11
6	Demuton Tanzania Ltd	3.06
7	Nachingwea Investment And Supplies Ltd	2.83
8	Daywinry Company Ltd	2.71
9	L. M. Malegeri Co Ltd	2.65
10	Pisah Limited	2.61
11	Pugna Agrifood Tanzania Ltd	2.50
12	Ahn & Raka Company Ltd	2.42
13	Jasaya General Trading Co Ltd	2.33
14	Splendors Control Ltd	2.27
15	Kiibale Company Ltd	2.00
16	I&R Agribusiness Company Ltd	1.96
17	Rahami Agri.Investment Limited	1.88
18	Kossa Company Limited	1.83
19	Kejuliana Co Ltd	1.63
20	Partner General Supplies	1.58
21	Chilindo Company Limited	1.38
22	Yuha Company Limited	1.29
<b>Wastani wa utendaji kwa ujumla</b>		<b>2.41</b>

#### **4.0. CHANGAMOTO**

#### **4.1. Waendesha Ghala Kutakiwa Kutoa Korosho Kama Walivyopokea:**

##### **4.1.1. Chimbuko**

*“Mwongozo Na.1 wa Usimamizi wa Masoko na Mauzo ya Korosho Ghafi wa Mwaka 2021/2022 Toleo la Kwanza”*, umeanisha taratibu za upokeaji, utunzaji na utoaji wa mazao katika Ghala Kuu unaotumiwa na Waendesha Ghala pamoja na wadau wengine. Aidha, katika msimu wa mwaka 2021/2022 utaratibu wa kusitisha uwekaji wa viwango vya unyaufu katika uliondolewa; na hivyo kuwataka Waendesha Ghala kutoa mizigo kulingana na uzito wa mazao ulioanishwa kwenye Stakabadhi ya Ghala bila kujali kiasi kinachopungua katika shughuli za uhifadhi kama vile ukataji sampuli, udhaifu wa vifungashio au mambo mengine yanayoweza kuasabisha upungufu kama ilivyotajwa katika Kiwango cha Korosho Ghafi (*Raw cashewnut-Specification*) Namba 2278 cha mwaka 2018 kama kiwango cha kitaifa (TZS 2278:2018) kilichotolewa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Uondoaji wa matumizi ya viwango vya upungufu ulitokana na kile kilichoonekana kwa baadhi ya Waendesha Ghala kutokuwa waaminifu kwa kuvitumia viwango hivyo kinyume na uhalisia, mfano katika eneo la Masasi lililoko ukanda bara ambapo kiwango cha upungufu wa uzito kilianishwa kuwa 0.69% ya mzigo uliopo endapo mzigo ungehifadhiwa ghalani katika kipindi cha siku 93; Mwendesha Ghala katika eneo husika wakati alipotoa korosho alikata upungufu wa asilimia 0.69% bila kujali uhalisia wa upungufu wa kila mzigo.

Hali hii ilipelekea baadhi ya wanunuzi kulalamikia kiwango hicho kilichokuwa kinatumika kuwa cha juu sana kuliko uhalisia; na katika baadhi ya vikao waliomba Serikali kupitia taasisi za utafiti na zile zenye mamlaka kufanya mapitio ya viwango hivyo ili kujiridhisha na uhalali wa viwango hivyo kutumika na kuja na mapendekezo ya viwango halisia.

Hivyo, kufuatia maagizo ya Serikali, Waendesha Ghala walitakiwa kupokea na kutoa korosho kwa uzito ule ule.

Katika msimu huu (2021/2022), Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) zilitekeleza Mwongozo mpya. Hata hivyo, katika utekelezaji wa Mwongozo WRRB imeendelea kupokea malalamiko kutoka kwa wanunuzi na Waendesha Ghala juu ya tofauti ya uzito kati ya kiasi kilichoingia na kutolewa kwa wanunuzi ikilinganishwa na stakabadhi husika.

Kufuatia hali hii Waendesha Ghala wamekuwa wakitoa mzigo kulingana na uzito ulioanishwa kwenye stakabadhi; na pale panapokuwa na upungufu wa uzito katika stakabadhi, inawalizimu Waendesha Ghala kuwafidia wanunuzi

upungufu wa uzito pale inapotokea. Fidia hii inalazimika kutoka katika uzito wa mzigo wa stakabadhi nyingine na kuweka kumbukumbu sahihi.

Kufuatia hali hiyo Bodi ilifanya ukaguzi mwanzo wa msimu na taarifa kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara (**Kiambatisho 6**).

#### **4.1.2. Visababishi vya upungufu wa uzito ghalani**

Kwa mujibu wa maandiko na uzoefu kutoka kwa wadau upungufu wa mazao ghalani unachangiwa na visababishi vifuatavyo.

**i. Mwongozo wa Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) kuwataka Waendesha Ghala kupokea mazao yenye unyevu wa hadi 10% (w/w) badala ya Kiwango cha Unyevu Msawazo (*Equilibrium Moisture Content*) cha 8.1% (w/w):**

Kutokana na takwa hilo la mwongozo, korosho huruhusiwa kupokelewa ghalani ikiwa na kiwango cha unyevu cha hadi 10% (w/w). Kulingana na maandiko ya kisayansi yanaonesha kuwa unyevu huo huendelea kupungua kutokana na sababu za kibailojia ikiwa ni pamoja na uhusiano kati ya hali ya unyevu angani (*humidity*), jotoridi (*temperature*), kiasi cha *iodine* na *peroksaidi* na mafuta kwenye korosho ghafi hadi kufikia kiwango msawazo cha asilimia 8.1% (w/w) (*Sabna et al, 2015*).

**ii. Uhaba wa ghala maeneo mengi:** Katika sekta ndogo ya korosho zinatumiwa ghala zenye ubora tofauti kuhifadhi korosho. Baadhi ya ghala zimejengwa mahususi kwa ajili ya kuhifadhi korosho na nyingine zimejengwa bila kuzingatia mahitaji maalum ya zao la korosho. Ghala hizi zinakua na mifumo tofauti ya kuingiza hewa na hata hali ya joto hubadilika kutokana na idadi ya vent za juu na chini, kimo cha ghala na idadi ya milango lliyopo. Pia, sehemu kubwa ya nchi haina ghala zenye viwango hivyo, hulazimika kuangalia vigezo vya msingi (*minimum requirement*) na kuzitumia. Sifa za msingi zinazozingatiwa ni pamoja na

- a. Kuta, bati, sakafu, milingo imara na madirisha ya kuingizia hewa (*venti*);
- b. Uwepo wa mizani iliyofanyiwa uhakiki na wakala wa vipimo Tanzania;
- c. Vipimia unyevu vilivyothibitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS);
- d. Vifaa vya kuzimia moto kama vile mitungi ya kuzimia na/au ndoo za mchanga;
- e. Upatikanaji wa mawasiliano ya simu na intaneti;
- f. Ukubwa wa kuhifadhi usiopungua kilogramu 200,000;

Hali hii ya miundombinu inaathari katika jotoridi na kiwango cha unyevu katika hewa ghalani.

- iii. **Wakulima kutumia gunia zenye viwango dhaifu:** Katika maeneo mbalimbali wakulima, Waendesha Ghala na wanunuzi wamekuwa wakilalamika kutokana na udhaifu wa vifungashio kwa kupasuka na kumwaga mazao ambayo husababisha upungufu mazao yaliyomwagika na kiasi kupotea wakati wa kurudishia kwenye vifungashio.



**Kielelezo: Gunia zilizopasuka licha ya kuwa ni mpya zinazosababisha umwagikaji ghalani**

- iv. **Uaminifu:** Baadhi ya wadau kuwa na vitendo vya kukosa uaminifu na kuiba mazao kwa makusudi kwa mfano
- **Mkulima:** Wajumbe kupunguza mazao wakati wa usafirishaji na kutoa taarifa kuwa ni unyaufu
  - **Mwendesha Ghala:** Kutokuwa makini katika kupokea unyevu, au kudokoa mazao yaliyo ghalani
  - **Wakala wa Mnunuzi:** Kupunguza uzito akiwa njiani kupeleka kwa mnunuzi na kudai kuwa ni unyaufu au kutokuwa makini kulinda mzigo wake na kuibiwa wakati wa usafirisha
- v. **Mabadiliko ya tabia ya nchi:** Katika kipindi cha karibuni pamekuwa na matukio ya mabadiliko ya tabia ya nchi ambapo kwa baadhi ya maeneo pamekuwa na ongezeko kubwa la joto ambalo husababisha madhara katika uhifadhi wa mizigo.

#### 4.1.3. Mapendekezo

Mapendekezo ya utatuzi wa changamoto ya upungufu mzigo ghalani;

- i. Bodi inashauri kufanyika tafiti katika mazao yanayotumia Mfumo na kuendelea kufanya mapitio kwa kila msimu.
- ii. Kushirikiana na kampuni za bima kuandaa viwango vya utendaji na namna ya ulipaji fidia unaoendana na viwango vya kimataifa.



- iii. Kuboresha miundombinu ya Usimamizi wa ghala ikiwemo kutumia mizani inayotoa taarifa za kieletroniki; kufanya kuwa lazima kila ghala kuwa na camera (CCTV), kuweka utambuzi wa kipekee wa kila gunia linalokuja ghalani na kuboresha teknolojia ya kushusha mizigo kwa kutumia *conveyors belt*.
- iv. Kufunga mizani ya kidijitali ambayo itatoa taarifa katika mifumo ya kompyuta kila kinachoingia na kutoka ili kuondoa uwezekano wa uchakachujaji taarifa;
- v. Kuboresha kanzidata itakayokuwa inawasiliana na wadau husika hususan wanunuzi pindi mzigo unapotoka ghalani kutuma taarifa ya kilogramu, gunia na ubora ili kupunguza uwezekano wa upunguzaji mzigo njiani.
- vi. Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuhakikisha uwepo wa vifaa vya kuhakiki ubora pamoja na kuzingatiwa kwa miongozo katika ngazi ya AMOCS;
- vii. Uhamasishaji wa ujenzi wa ghala bora na kisasa zenye kupunguza changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa na miundombinu bora ya uhifadhi.

#### **4.2. Changamoto Nyingine**

- a. Uelewa mdogo wa wadau majukumu na mipaka ya Bodi na taasisi nyingine katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala;
- b. Uelewa mdogo juu ya jinsi Mfumo unavyofanya kazi;
- c. Kutozingatiwa kwa viwango vya ubora kwa baadhi ya wadau hususan wakati wa kuandaa mazao kabla hayajafikishwa ghalani;
- d. Baadhi ya wadau kutotoa ushirikiano wa kutosha kutatua changamoto za kimfumo hususan kwenye tafiti za kuboresha utendaji;
- e. Uhitaji wa kufanyie marejeo ya *lien* ya Sh.38 kutokidhi Gharama za sasa;

## Kiambatisho Na.1

N	Top Depositors (Kg)	Top Grade I	Top Average Revenue	Mkoa	Wilaya	AMCOS	Received (Kg)	Grade I (Kg)	Grade II (Kg)	SOT	Moisture (%w/w)	Nut Count	Average	Max	Min	(Tsh)
1	432	417	439	Lindi	Kilwa	Jaribuni Amcos Ltd	200,288	200,288	-	49.76	8.9	179	1,995.95	2,130.00	1,700.00	402,773,854.00
2	656	638	654	Lindi	Kilwa	Kingoli Amcos Ltd	41,232	41,232	-	51.03	9.1	177	2,082.50	2,120.00	2,010.00	86,217,860.00
3	563	552	563	Lindi	Kilwa	Kinjumbi Amcos Ltd	93,420	93,420	-	49.51	8.9	183	2,028.71	2,100.00	1,960.00	189,857,340.00
4	669	646	669	Lindi	Kilwa	Linali Amcos Ltd	36,421	36,421	-	50.35	8.5	195	2,020.00	2,100.00	1,960.00	73,765,490.00
5	318	307	330	Lindi	Kilwa	Matandu Amcos Ltd	297,325	296,994	331.00	49.78	8.4	193	2,002.33	2,130.00	1,635.00	598,425,363.00
6	85	86	93	Lindi	Kilwa	Mshikamano Amcos Ltd	616,040	605,702	10,338.00	49.73	8.7	181	2,055.22	2,275.00	1,635.00	1,265,784,095.00
7	149	161	158	Lindi	Kilwa	Mtungi Amcos Ltd	498,779	475,783	22,996.00	49.85	9.1	182	2,031.10	2,100.00	1,601.00	1,011,683,415.00
8	233	222	231	Lindi	Kilwa	Namakongoro Amcos Ltd	385,546	385,546	-	49.84	9.4	181	2,041.58	2,130.00	1,601.00	787,418,559.00
9	262	252	265	Lindi	Kilwa	Nang'Oo Amcos Ltd	349,972	349,972	-	50.36	8.8	174	2,043.26	2,120.00	1,960.00	714,539,118.00
10	36	35	38	Lindi	Kilwa	Pande Amcos Ltd	821,590	821,590	-	50.17	9.3	178	2,078.40	2,275.00	1,960.00	1,705,797,443.00
11	279	290	290	Lindi	Kilwa	Ruyaya Amcos Ltd	330,752	320,278	10,474.00	49.38	8.8	185	2,032.80	2,100.00	1,601.00	671,783,179.00
12	155	148	160	Lindi	Kilwa	Sisi Kwa Sisi Amcos Ltd	492,133	492,133	-	49.80	9.0	179	2,038.08	2,275.00	1,700.00	1,002,677,800.00
13	407	396	404	Lindi	Kilwa	Somanga Amcos Ltd	222,060	220,773	1,287.00	49.81	8.6	184	2,052.96	2,275.00	1,635.00	459,563,096.00
14	290	276	296	Lindi	Kilwa	Tapwa Amcos Ltd	322,641	322,641	-	50.27	8.7	188	2,049.18	2,275.00	1,700.00	663,443,899.00
15	582	565	579	Lindi	Kilwa	Ukangala Amcos Ltd	82,417	82,417	-	50.19	8.2	196	2,047.63	2,100.00	2,001.00	168,884,408.00
16	198	215	205	Lindi	Kilwa	Ulina Amcos Amcos Ltd	429,906	394,144	35,762.00	49.94	9.3	178	2,038.91	2,130.00	1,601.00	875,589,110.00
17	54	50	57	Lindi	Kilwa	Umoja Mikoma Amcos Ltd	721,926	721,926	-	49.92	9.2	175	2,035.82	2,130.00	1,960.00	1,469,947,666.00
18	480	482	479	Lindi	Lindi	Chikonji Amcos Amcos Ltd	156,436	148,280	8,156.00	49.24	9.0	179	2,062.59	2,200.00	1,640.00	323,783,140.00
19	733	699	730	Lindi	Lindi	Kingoli Amcos Ltd	16,800	16,800	-	50.00	8.7	184	2,070.00	2,070.00	2,070.00	34,776,000.00
20	171	168	174	Lindi	Lindi	Kitumiki Amcos Ltd	458,990	443,781	15,209.00	49.26	8.9	177	2,110.98	2,286.00	1,640.00	976,437,649.00
21	510	503	504	Lindi	Lindi	Mchinga Amcos Ltd	136,248	131,501	4,747.00	49.17	8.7	178	2,079.58	2,205.00	1,640.00	288,506,290.00
22	674	650	672	Lindi	Lindi	Milola Amcos Ltd	35,237	35,237	-	49.60	8.8	183	2,030.80	2,052.00	2,002.00	71,391,004.00
23	436	422	437	Lindi	Lindi	Mnali Amcos Amcos Ltd	197,549	197,549	-	49.80	9.1	177	2,071.10	2,205.00	1,960.00	409,257,486.00
24	105	108	110	Lindi	Lindi	Mnazimmoja Amcos Amcos Ltd	578,625	557,360	21,265.00	49.23	8.7	178	2,098.55	2,286.00	1,640.00	1,195,130,351.00
25	691	666	677	Lindi	Lindi	Mnolea Amcos Ltd	30,025	30,025	-	50.00	9.8	196	2,200.00	2,200.00	2,200.00	66,055,000.00
26	692	667	690	Lindi	Lindi	Mtungi Amcos Ltd	29,914	29,914	-	49.00	9.1	183	2,030.00	2,050.00	2,010.00	60,726,020.00
27	640	620	623	Lindi	Lindi	Muungano Amcos Ltd	54,300	54,300	-	48.25	9.4	183	2,165.00	2,250.00	2,010.00	118,636,650.00
28	232	236	224	Lindi	Lindi	Mvuleni Amcos Ltd	386,323	365,457	20,866.00	48.37	8.8	176	2,114.47	2,250.00	1,601.00	802,614,135.00
29	523	518	516	Lindi	Lindi	Nachunyu Amcos Ltd	119,384	119,384	-	49.30	8.1	183	2,207.20	2,286.00	2,040.00	263,972,652.00
30	449	441	448	Lindi	Lindi	Naki Amcos Ltd	184,207	184,207	-	50.16	8.5	192	2,047.16	2,250.00	1,960.00	377,091,224.00
31	762	730	761	Lindi	Lindi	Namakongoro Amcos Ltd	10,055	10,055	-	50.00	8.5	181	2,010.00	2,010.00	2,010.00	20,210,550.00
32	450	447	451	Lindi	Lindi	Nangaru Amcos Ltd	182,908	176,272	6,636.00	49.18	9.6	179	1,994.47	2,250.00	1,640.00	367,586,570.00
33	570	570	566	Lindi	Lindi	Natam Amcos Ltd	90,125	80,190	9,935.00	48.89	8.6	172	2,063.00	2,210.00	1,601.00	185,945,525.00
34	316	339	321	Lindi	Lindi	Navanga Amcos Ltd	298,829	273,549	25,280.00	49.41	9.2	176	2,058.00	2,250.00	1,640.00	618,869,480.00
35	394	401	384	Lindi	Lindi	Ng'Apa Amcos Ltd	241,711	218,383	23,328.00	48.76	8.9	179	2,038.52	2,205.00	1,640.00	498,532,405.00
36	554	540	548	Lindi	Lindi	Pachani Amcos Ltd	99,797	99,797	-	49.50	8.8	178	2,098.70	2,205.00	2,002.00	209,497,001.00
37	645	628	640	Lindi	Lindi	Pangatena Amcos Ltd	50,195	50,195	-	49.20	9.5	171	2,091.00	2,205.00	2,010.00	104,952,925.00
38	304	327	314	Lindi	Lindi	Rutamba Amcos Ltd	310,888	280,689	30,199.00	48.10	9.5	179	2,008.47	2,250.00	1,640.00	630,787,385.00
39	590	587	585	Lindi	Lindi	Sudi Amcos Ltd	78,281	70,135	8,146.00	48.75	9.1	176	2,051.25	2,205.00	1,640.00	161,338,490.00
40	63	62	59	Lindi	Lindi	Ujirani Mwema Amcos Ltd	691,680	673,579	18,101.00	48.98	8.9	185	2,109.87	2,286.00	1,601.00	1,461,212,266.00
41	688	662	686	Lindi	Lindi	Ukombozi Nakiu Amcos Ltd	31,128	31,128	-	49.00	8.7	190	1,985.00	2,010.00	1,960.00	62,104,630.00
42	206	195	209	Lindi	Lindi	Ulina Amcos Amcos Ltd	424,079	424,079	-	48.93	8.6	180	2,031.86	2,200.00	1,960.00	860,395,100.00
43	38	43	46	Lindi	Lindi Vijijini	Kiwalala Amcos Ltd	795,824	753,838	41,986.00	48.96	9.0	178	2,080.53	2,200.00	1,640.00	1,584,989,746.00
44	362	348	358	Lindi	Lindi Vijijini	Malungo Amcos Ltd	263,640	263,640	-	50.30	9.1	150	2,111.75	2,275.00	2,021.00	556,273,986.00
45	109	110	121	Lindi	Lindi Vijijini	Mandwanga Amcos Ltd	570,485	550,812	19,673.00	48.60	9.2	154	2,057.36	2,260.00	1,640.00	1,153,233,100.00
46	757	726	751	Lindi	Lindi Vijijini	Matama Amcos Ltd	11,240	11,240	-	49.80	8.7	190	2,080.00	2,080.00	2,080.00	23,379,200.00
47	240	234	229	Lindi	Lindi Vijijini	Mmangawanga Amcos Ltd	379,522	369,001	10,521.00	48.86	9.2	177	2,085.71	2,275.00	1,640.00	791,882,077.00
48	168	183	191	Lindi	Lindi Vijijini	Mnolea Amcos Ltd	462,391	437,524	24,867.00	48.96	8.6	183	2,062.00	2,275.00	1,708.00	910,665,998.00
49	115	109	123	Lindi	Lindi Vijijini	Mtama Amcos Ltd	551,667	551,667	-	49.91	8.7	180	2,086.42	2,275.00	1,700.00	1,132,970,043.00
50	182	206	192	Lindi	Lindi Vijijini	Mtua Amcos Ltd	443,711	406,953	36,758.00	48.86	9.1	177	2,042.00	2,275.00	1,640.00	908,220,515.00
51	42	39	40	Lindi	Lindi Vijijini	Nachunyu Amcos Ltd	769,638	761,422	8,216.00	49.69	8.8	175	2,155.25	2,275.00	1,710.00	1,661,542,068.00
52	258	253	270	Lindi	Lindi Vijijini	Nahukahuka Amcos Ltd	354,548	344,560	9,988.00	48.89	9.4	160	2,039.50	2,260.00	1,700.00	703,428,397.00
53	302	302	302	Lindi	Lindi Vijijini	Namangale Amcos	309,638	309,638	-	50.57	8.5	183	2,082.60	2,275.00	1,700.00	645,571,611.00
54	395	380	388	Lindi	Lindi Vijijini	Nanyum Amcos Ltd	240,956	240,956	-	50.63	9.0	169	2,043.88	2,201.00	1,700.00	493,126,671.00
55	89	83	83	Lindi	Lindi Vijijini	Natam Amcos Ltd	610,150	600,116	10,034.00	49.67	8.8	169	2,142.18	2,275.00	1,710.00	1,306,973,998.00
56	367	355	357	Lindi	Lindi Vijijini	Navanga Amcos Ltd	260,045	260,045	-	50.43	8.9	174	2,163.46	2,275.00	2,021.00	562,623,015.00
57	292	306	295	Lindi	Lindi Vijijini	Nyangamara Amcos Ltd	321,420	298,408	23,012.00	48.84	9.4	169	2,062.03	2,210.00	1,710.00	663,561,768.00
58	39	37	42	Lindi	Lindi Vijijini	Nyangao Amcos Ltd	795,285	795,285	-	49.83	8.7	178	2,021.77	2,275.00	1,700.00	1,602,228,378.00
59	49	45	55	Lindi	Lindi Vijijini	Nyengedi Amcos Ltd	744,270	744,270	-	49.84	8.8	179	2,092.63	2,275.00	1,700.00	1,509,602,295.00
60	339	364	352	Lindi	Lindi Vijijini	Pangatena Amcos Ltd	280,861	252,597	28,264.00	48.47	9.1	175	2,023.59	2,275.00	1,600.00	570,452,365.00
61	188	180	182	Lindi	Lindi Vijijini	Sudi Amcos Ltd	439,106	439,106	-	49.96	8.8	171	2,115.90	2,275.00	2,025.00	930,714,191.00
